TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA



FAIDA ZA MAFUTA "MWALI" YA NAZI (Virgin Coconut Oil-VCO)

UTANGULIZI

- ✓ Mafuta mwali (Virgin Coconut Oil-VCO) ni mafuta yatokanayo na nazi ambayo hayajaongezwa kemikali yoyote wala kuchemshwa; hukamuliwa, huchujwa na kufungashwa
- ✓ Hukamuliwa toka kwenye nazi safi, kwa mfumo wa Cold Press hivyo ni asili kwa asilimia mia (100%)
- ✓ Pamoja na kuwa na ladha nzuri ya asili, pia yana virutubisho vifuatavyo: Lauric acid, capric acid, caprylic acid, myristic acid, palmitic, Choline, vitamin E, K and Iron. Lauric acid, capric acid na caprylic super fatty acids
- ✓ 50% ya fatty acid iliyo kwenye mafuta mwali ya nazi ni lauric acid hubadilishwa na mwili kuwa monolaurin ambayo hupatikana katika maziwa ya binadamu (mama)



Picha 1. Ukamuaji wa mafuta mwali ya nazi

MATUMIZI YA MAFUTA MWALI YA NAZI

- ✓ Mafuta mwali ya nazi yanatumika kwa chakula kama kunywa, kuweka kwenye saladi, kupikia, kuokea, na kukaangia
- ✓ Mafuta ya Nazi ni kipenzi cha Watoto wachanga husaidia kutibu magonjwa ya Ngozi kama Eczema, kuwashwa na kulainisha ngozi
- ✓ Ni mali ghafi ya viwandani kwa kutengeneza sabuni, mafuta ya kujipaka na vipodozi



Picha 2. Mafuta hukamuliwa kutoka kwenye nazi bora na zilizokomaa vizuri

FAIDA YA MAFUTA MWALI YA NAZI KWA AFYA

- ✓ Huimarisha kinga ya mwili na afya ya Ngozi
- ✓ Mazuri kwa afya ya ubongo: Huongeza kumbukumbu na ubongo kufanya kazi vizuri
- ✓ Yanaharakisha mmeng'enyo wa chakula
- ✓ Hupunguza lehemu (Cholestorol) mbaya mwilini na mafuta mabaya


- ✓ Yana ukinzani dhidi ya vimelea (Antimicrobial effects) vishambuliavyo mwili
- ✓ Antioksidanti
- ✓ Hufanya usizeeke haraka na huondoa uchovu
- ✓ Hutumika kwa kuchua viungo na kusinga

FAIDA ZA UONGEZAJI THAMANI WA ZAO LA NAZI KUPITIA MAFUTA MWALI

- ✓ Ukamuaji wa mafuta mwali humuongezea faida Mkulima mara 5 hadi 8 kulinganisha na kuuza mbata, madafu hata nazi ghafi za kupikia
- ✓ Uuzaji wa makapi/machicha pia huongeza faida kwani ni chakula muhimu cha Mifugo



Picha 3. Uchujaji wa mafuta kabla ya kufungasha kwenye chupa



Picha 4. Nazi iliyokomaa kwa ajili ya ukamuaji wa mafuta ya mwali



Picha 5. Mnazi uliokomaa ukiwa Shambani



Picha 6. Nywele zenye afya kutokana na Matumizi ya Mafuta Mwali ya Nazi

MATUMIZI YA MAFUTA MWALI YA NAZI KWA KUJIPAKA

- ✓ Huzifanya nywele kuwa na afya na ukuaji bora. Matumizi kwenye nywele hukabiliana na mba, chawa na mayai yake
- ✓ Hukabili baadhi ya magonjwa ya ngozi (psoriasis, eczema, dermatitis), huilinda isipauke na kukabili makunyanzi na ngozi kutepeta
- ✓ Ni mazuri zaidi kwa kupaka watoto wachanga

Kwa ushauri wasiliana na Meneja
Kituo cha Utafiti wa Kilimo Mikocheni

+255 (0) 22 2700552
+255 (0) 676692467
Barabara ya Coca Cola,
Kitalu Na.22, Dar es Salaam,
Barua pepe: cmmikocheni@tari.go.tz